**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

**SIMU**
0787-303467 – MKUU WA SHULE
0768-976221 – MAKAMU MKUU WA SHULE
0755-572155 – MAKAMU MKUU WA SHULE

S.L.P 345
**MARANGU**
Tarehe …………….

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA ASHIRA WILAYA YA MOSHI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA …………..**

## UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Ashira, kidato cha Tano (V) Tahasusi (combination) ya HGE/CBG/EGM/HKL/HGL/HGFa na HGLi kwa mwaka wa masomo ……………...
Unategemewa kuwa utakuwa mwanafunzi mwadilifu, mwenye nidhamu, juhudi, maarifa na utakayeonyesha ushirikiano mkubwa kwa watumishi pamoja na wanafunzi wenzako kwa muda wote. Utatakiwa kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule. Kwa kufanya hivyo utaweza kutimiza malengo yako, ya wazazi/walezi na serikali kwa ujumla.
Shule ni ya bweni kwa wasichana, ipo wilaya ya Moshi Vijijini umbali wa km. 45.5 kutoka Stendi kuu ya mabasi ya Moshi Mjini. Kutoka Moshi Mjini hadi Marangu Mtoni utapanda mabasi yaendayo Mwika au Kilema kwa nauli ya shilingi 2,500/= (elfu mbili mia tano tu). Shuka Marangu Mtoni. Chukua taxi kwa nauli ya shilingi 4,000/= (elfu nne tu) au pikipiki kwa shilingi 1,500/= (elfu moja mia tano tu) hadi shuleni ambapo ni km 1.5 tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ……………Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………. iliyopangwa na serikali. Tafadhali njoo na "**Hati ya Matokeo halisi**" **(Original Result Slip).**

### 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1 SARE YA SHULE

i. Aje na sketi mbili ndefu na Bolero mbili aina ya Takroni Dark Blue, sketi iwe ndefu ifike kwenye kifundo cha miguu.
ii. Mashati mawili (2) meupe ya tetroni ya mikono mifupi atawekewa nembo akifika shuleni.
iii. Aje na Sweta (2) mbili rangi ya Dark Blue yenye shingo **V** isiyo na vifungo.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga kwa kamba (gidamu) vinavyofunika miguu na visiwe na visigino (flat sole) pia visiwe na shingo ndefu.
v. Soksi nyeupe ndefu (stockings) jozi nne (4) zisizo na urembo zinazifika kwenye goti kwa ajili ya sare ya shule.
vi. Wanafunzi wa Kiislamu waje na Hijabu mbili nyeupe na moja ya rangi ya dark blue ambayo inafanana na rangi ya sketi ifike kwenye kiwiko cha mkono (elbow).
vii. Aje na pulneck mbili (2) nyeupe ya mikono mirefu kwa ajili ya kujikinga na baridi.
viii. Aje na Tracksuit mbili (2) rangi ya Dark Blue aina ya Adidas au Puma yenye mistari mieupe kwenye mikono na pembeni mwa suruali isiwe na kofia, kwa ajili ya kuvaa wakati wa usiku (evening preparation) kwa ajili ya baridi na kuzuia kuumwa na mbu.
ix. Nguo ya kazi (working dress) gauni aina ya Takron Dark Blue kitambaa kinafanana na sketi.
x. Nguo za michezo; Bukta , T-shirt (jezi) rangi nyeupe na soksi ndefu za rangi nyekundu pamoja na raba nyeusi kwa ajili ya michezo.
xi. Tshirt mbili (2) ambazo zitawekwa nembo ya shule zitapatikana shuleni mzazi atagharamia wakati mwanafunzi atakaporipoti shuleni.
**xii. Angalizo: Nguo za nyumbani haziruhusiwi Shuleni.**

## 2.2. MICHANGO MBALIMBALI

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. . | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya Tshs. 20,000/=kwa mwaka na malipo hayo yalipwe kwenye akaunti ya shule.

**Kumbuka:** Fedha zote zilipwe kabla ya mwanafunzi kufika shuleni katika Benki ya NMB jina la akaunti **Ashira Girl's Secondary School Account number 40301200159 uje na "Bank Paying Slip".** Tafadhali andika jina la Mwanafunzi, kidato na tahasusi. Fedha zote zinaweza kulipwa katika Benki ya NMB Tawi lolote lililo karibu kwa jina la akaunti ya Shule iliyotajwa hapo juu. Tafadhali leta Bank Pay in Slip halisi kwa ajili ya uthibitisho wa malipo. Pia ni vizuri ukaitoa (photocopy) Mzazi/mlezi ukabaki nayo kwa ajili ya kumbukumbu zako.

**MUHIMU:**
Fedha taslimu hazitapokelewa Shuleni kwa sababu za kiusalama. Kabidhi **"Bank-Pay-in slip** kwa Mwalimu atakayekupokea.

**2.3. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Aje na Sanduku imara la chuma (tranka).
ii. Mashuka jozi mbili (02) rangi ya pinki iliyokolea, mto mmoja(01) na foronya zake rangi ya pinki.
iii. Blanketi moja zito kwa ajili ya baridi.i
iv. Aje na chandarua nyeupe kwa ajili ya kujikinga na mbu.
v. Aje na nguo ya kulala usiku nzito (Night dress/pajama) rangi ya pinki au nyeupe.
vi. Yebo nyeusi zisizo na urembo kwa ajili ya kushindia na kuogea.
vii. Vifaa vya usafi wa mwili, dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kupaka, sabuni ya kuogea na kufulia, kitana, rangi ya viatu, brashi, taulo, nguo za ndani za kutosha, ndoo moja (01) ndogo (lita kumi) na kikombe cha kuogea (lita moja).
viii. Chupa ya maji ya kunywa.
ix. Saa ya mkononi ni muhimu sana.
x. Mwavuli /koti la mvua (rain coat).
xi. Tochi (01) ndogo inayotumia betri siyo umeme.
xii. Vyombo vya kulia chakula chakula (sahani, kijiko, bakuli, kikombe) vitanunuliwa kwenye duka la shule. Asije navyo tafadhali.

**MUHIMU:**

(i) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vya DINI yake husika akiwepo shuleni. Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kubadilisha DINI/DHEHEBU akiwepo shuleni bila idhini ya mzazi kwa maandishi. Vitabu vya dini kwa ajili ya sala na vipindi vya dini hapa shuleni ni kama inavyoonesha:-

- Waislamu - Njoo na Quran Tukufu.
- Wakatoliki - Njoo na Misale ya Waumini, Biblia na Rozari.
- Waprotestant chini ya CCT – walete Biblia na Mwimbieni bwana/Tumwabudu Mungu.

Madhehebu mengine ya Kikristo njoo na Biblia na vitabu vya nyimbo kwa mujibu wa imani yako. Mfano Wasabato, Pentekoste n.k.

## (ii) Fedha za matumizi (pocket money)

Mzazi/Mlezi umpe mwanao fedha za matumizi kiasi cha kuridhisha kulingana na uwezo wa mzazi/mlezi.
Ushauri epuka kumpa mwanao fedha nyingi mno kwani zinaweza kuwa kichocheo cha wizi hapa shuleni pia mwanao kuwa na tabia ya majivuno ambayo siyo nzuri.

## 2.4. VIFAA VYA MAFUNZO

### a) VIFAA VYA KUJIFUNZIA

(i) Aje na madaftari makubwa (counter books) kumi (10) (three quire)

(ii) Aje na ream (A4) mbili kwa mwaka kwa tahasusi ya CBG,EGM, HGL, HGE,HKL, HGLi na kwa wanafunzi wa HGFa waje na Ream (A3) (karatasi pana) mbili (02) kwa mwaka.

(iii) Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma tahasusi ya EGM, CBG na HGE.

(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology.

(v) Aje na koti la maabara (lab coat) nyeupe kwa wanafunzi wa science.

(vi) Aje na stop watch kwa wanafunzi wa science.

(vii) Kamusi ya Kiingereza Oxford Advanced Learner’s Dictionary kwa wanafunzi wote

(viii) Aje na jalada (file) mbili moja kwa ajili ya nyaraka zake na binafsi nyingine kwa ajili ya mitihani.

(ix) Aje na stapler machine moja (01) na staple pins kwa matumizi binafsi.

(x) Begi la kubebea madaftari la kubeba mgongoni.

(xi) Graph paper kwa matumizi binafsi kwa wote isipokuwa kwa tahasusi ya HKL.

### b) VITABU

Mzazi/mlezi unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na tahasusi yake ili kumpa mwanafunzi uhuru wa kujisomea bila kutegemea vilivyopo vya kushirikiana. Nakala ya vitabu imeambatanishwa, Kama inavyoonyeshwa katika ukurasa wa 14, 15 na 16.

**VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA:**

**Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi wa mazingira ya Shule.**

A. **WANAFUNZI WOTE :** wanatakiwa kuja na sabuni ya maji (Disinfectant ya DEXI) lita 5, fagio za chelewa 2 wenye mpini 1 na usio na mpini 1 na ndoo mbili moja kubwa na moja ndogo za plastic lita (10/20).

B. **Wanafunzi wote wa EGM :** Waje na hard broom, soft broom, toilet brush, kijembe kidogo chenye pande mbili za rato na mundu (sicke) kifaa cha kukatia majani chenye makali.

C. **Wanafunzi wote wa HGL** - Waje na Drying Mopper (dekio la nyuzi na ndoo yake), soft broom, hard broom, toilet brush na kikopo chake, squizer na reki.

D. **Wanafunzi wote wa HGE**. _ Waje na mundu (sickle), hard Broom, soft broom, toilet brush na kikopo chake, panga, fyekeo na squizer.

E. W**anafunzi wote wa CBG**. _ Walete Rato, Hard Broom, Soft Broom, toilet brush na kikopo chake, jembe na mpini wake na fyekeo.

F. **Wanafunzi wa HKL.** – Mfagio wa buibui 1 wenye mpini mrefu, (cobweb broom), panga, jembe na mpini wake, soft broom, hard broom, toilet brush na kikopo chake na fyekeo.

**Wanafunzi wa HGFa** – Mundu (sickle) - kifaa cha kukatia majani chenye makali, hard broom, soft broom, toilet brush na kikopo chake, reki na fyekeo.

**Wanafunzi wa HGLi -** Panga, Fyekeo, soft broom, Hard broom, reki, toilet brush na kikopo chake, jembe na mpini wake na squizer.

Kabidhi vifaa hivi kwa mwalimu atakayekupokea. Tafadhali mzazi/mlezi binti yako alete vifaa husika.

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni. KUJITUMA, KUJITAMBUA, IBADA NA NIDHAMU ni misingi mikubwa ya shule yetu, hivyo haya ni ya muhimu kuyaishi ukiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Ashira.

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule.**

i. Malengo ya shule ni ufaulu wa daraja la kwanza tu. Hivyo utatakiwa kusoma kwa bidii kutimiza malengo hayo yaliyokusudiwa.
ii. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
iii. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule.
iv. Kushiriki clubs za masomo na kijamii na michezo ni lazima.
v. Kuhudhuria kikamilifu masomo ya usiku (preparation).
vi. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa ambazo ni halali.
vii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii. Kutoka bila ruhusa utaadhibiwa na utalazimika kuchangia tofali 100 kuchangia kujenga ukuta wa shule.
viii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.
ix. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa ukiwa shuleni, ukipata kibali cha kutoka nje ya shule au ukiwa safarini wakati wa likizo ndefu/fupi.
x. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.
xi. Kutunza mali za shule.
xii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xiii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shulenikwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marukuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**
- ❖ **Manukato na vipodozi vya aina yoyote ile haviruhusiwi shuleni..**

## 3.2.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE:

1. Wizi.
2. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
3. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule
6. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
7. Uasherati na uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
8. Ubakaji.
9. Ulevi wa pombe, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara.
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
11. Kudharau bendera ya taifa.
12. Kusababisha, kupata mimba, kuharibu mimba au kutoa mimba ndani na nje ya shule.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Mwanafunzi kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi ama vifaa vinavyohusiana na simu akiwa shuleni, na vifaa vingine vya umeme mfano radio, pasi nk.
15. Ni marufuku kuvaa bangili, hereni, mikufu, kupaka rangi za kucha, lipstick, kupaka wanja na kutinda nyusi.
16. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
17. Kufuga ndevu.
18. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.

**NIDHAMU NI MSINGI WA KUTIMIZA MALENGO YAKO UKIWA ASHIRA SEKONDARI.**

**NB.** Maamuzi ya makosa haya hayatahitaji mzazi kujulishwa zaidi ya mara moja ili kutimiza adhabu ya kumsimamisha sgule mwanafunzi. Ni wajibu wa mwanafunzi kuishi na kufuata taratibu zote za shule. Mzazi/mlezi/shirika/mfadhili na mwanafunzi, soma na kuzielewa sheria zote za shule na kuzikubali kwa kusaini fomu ya makubaliano ya utii.

## 4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

A. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu hospitali ya Serikali. Mzazi/mlezi hakikisha umempima mtoto wako kikamilifu.

B. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.

C. Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

D. Alete picha 4 (Passport size) za Wazazi/Walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

N.B Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA ASHIRA SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule……………………………..**

**Jina la Mkuu wa Shule ZAINABU S. SHESHUI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule……………………………**

**N.B kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

**Z. S. SHESHUI**
**MKUU WA SHULE**

# ASHIRA SEKONDARI


AINA YA KITAMBAA CHA SKETI, BOLERO NA NGUO YA KAZI NI DARK BLUE


RANGI YA KITAMBAA CHA SARE YA SHULE INAFANANA NA SURUALI ZA TRAFIC POLICE WANAWAKE WA TANZANIA.

**A: SKETI:**
Zipu iwe ya pembeni siyo ya nyuma. Marinda ya sketi yaelekee upande mmoja. Marinda jumla yawe 12 Sketi iwe ndefu inayofikia vifundo vya miguu


**B: SWETA**
Rangi darkblue
Shingo ya "V" mbele

**C: Nguo ya kazi** (working dress)
mshono ni shifti isiyo ya kubana Gauni iwe ndefu inayofika vifundo vya miguu






**D: BOLERO**



Haina vifungo wala zipu urefu wa bolero ufike usawa wa pindo (belt) la sketi.

**E. SICKLE (MUNDU)**



**FOMU A**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL AEMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Ashira Girls Secondary School,
P.O. Box 345,
**MARANGU.**

Tarehe …………...

The Medical Officer
**GOVERNMENT HOSPITAL.**

Name of pupil________________________________________________________________
Please examine the above named pupils and arrange any necessary treatment so that Certificate can be signed and the pupil can return it in time for the beginning of next term.

**MEDICAL CERTIFICATE (To be filled by Medical Officer).**
I have Examined the above named with regard to
REMARKS:-
Skin_____________________________________________
Eyes_____________________________________________
Ears______________________________________________
Tooth/teeth_______________________________________
Blood____________________________________________
Pressure__________________________________________
Abdomen_________________________________________
Urine_____________________________________________
Stool______________________________________________
HB Hemoglobin_____________________________________
Any disabilities _____________________________________
TB ______________________________________________
And consider that

(1) The pupil is in good health free from infections disease, worms, and bilharzias and is fit to return to school.
(2) She is now fit to return to school after being treated for
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________

Name and signature of Medical Officer___________________________________
Date______________________________________________________________

**FOMU B**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU**.

Kumb. Na. ASH/S/24/58 20 Mei, 2026.

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI – MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI**

Sehemu A: Ijazwe na mwanafunzi
(1)Jina la mwanafunzi (majina matatu)______________________________________________
______________________________________________________________________
(2) Taifa______________________________________________________________
(3)Tarehe ya kuzaliwa____________________________________________________
(4) Dini______________________________________________________________
(5) Shule anayotoka_____________________________________________________
Tarehe ya kutoka Shule__________________________________________________

**SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

(1) Jina la mzazi/mlezi(majina matatu)
______________________________________________________________
(2) Mahali unapoishi Kata______________________________Kijiji______________________
(3) Anuani ya mzazi/mlezi__________________________________Namba ya simu__________
(4) Kazi ya mzazi/mlezi____________________________Mahali anapofanya kazi na anwani
______________________________________________________________

Ndugu wawili wa karibu (unaowaelewa badala ya mzazi/mlezi):-

(a) Jina_________________________________________________________
Anwani_________________________________________________________
Simu namba_____________________________________________________
Uhusiano wake na mzazi/mlezi______________________________________

(b)Jina__________________________________________________________
Anwani_________________________________________________________
Simu namba_____________________________________________________
Uhusiano wake na mzazi/mlezi______________________________________

Jina la mzazi/mlezi_________________________________________________
Tarehe__________________________________________________________
Sahihi__________________________________________________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HATI YA MAKUBALIANO YA KUFUATA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

**FOMU C**

Shule ya Sekondari Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU**.

Tarehe …………..

### AHADI YA MWANAFUZI

Mimi mwanafunzi (majina matatu) ____________________________________________
____________________________________________________________________________
Ninaahidi kufuata taratibu na sheria zote za shule ikiwa ni pamoja na kutokushiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Ninaweka ahadi ya kuwa mwanafunzi mtiifu kwa walimu, serikali ya wanafunzi, na wote wanaowajibika nami

Saini________________________________________Tarehe__________________________

### AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi mzaz/mlezi mwanafunzi_____________________________________________________
Kidato cha tano__________________________________mwaka________________________
Ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwa kipindi chote mwanangu atakachokuwa katika shule ya Ashira Sekondari.

Jina la mzazi/mlezi______________________________________Saini_________________

Tarehe_________________________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**FOMU D**

**ANWANI**

**MAJINA YA WAZAZI/WALEZI WANAOTAMBULISHWA SHULENI.**
**Alete picha nne passportsize za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa karibu na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu**

1.Jina ………………………………… UHUSIANO …………
NAMBA ya simu ……………………/……………………..
Namba ya NIDA …………………………………………...
SAINI ………………………… TAREHE …………………..

2.Jina ………………………………… UHUSIANO …………
NAMBA ya simu ……………………/……………………..
Namba ya NIDA …………………………………………...
SAINI ………………………… TAREHE …………………..

3.Jina ………………………………… UHUSIANO …………
NAMBA ya simu ……………………/……………………..
Namba ya NIDA …………………………………………...
SAINI ………………………… TAREHE …………………..

4.Jina ………………………………… UHUSIANO …………
NAMBA ya simu ……………………/……………………..
Namba ya NIDA …………………………………………...
SAINI ………………………… TAREHE …………………..

**HISTORY**

1. Basic facts About the World History (New syllabus 2025) By Comrade Shibitali Tumaini. C.K.
2. The Solutions guide to A-level History form five new syllabus (fully Solved) by Haruna Mazenza.

3. History for Advanced Secondary schools Student's book form Five by Tanzania Institute of Education (TIE)

**BIOLOGY**

1. New Understanding Biology for Advanced Level (4$^{th}$ Edition) by Glenn and Suzan Toole.
2. Guide to Dissection by H.G.Q Rowert.
3. Biology for Advanced level by TIE.

**GEOGRAPHY**

1. Physical Geography for Secondary School (by TIE) form Five and Six.
2. Practical Geography for Advanced Secondary Schools by (TIE) form Five and Six Student books.
3. Principples of physical Geography - by F. J….Monk house.
4. Land forms 1. Africa – An Introduction to Geomorphology – by Colin Buckle.
5. Africa – by J.M Prichard.
6. A comprehensive Approach physical Geography for SecondarySchool by D.T Msabila.
7. Physical Geography by Charles Plummer.
8. Foundation of Physical Geography by B. Michael.
9. Human and Economic Geography – by Gohcheng & Morgan.

**ENGLISH LANGUAGE**

1. English For Advanced Secondary Schools Student's Book Form Five.
2. English For Advanced Secondary Schools Student's Book Form Six.

**READINGS FOR ENGLISH LANGUAGES**
**NOVELS**
1. Animal Farm by George Orwel.
2. Chasing the Leopard, Finding the Lion by Julie Wakeman – Linn

**PLAYS**

1. The Government Inspector by Nikolai V Gogol
2. A taste of Heaven by Farouk Topan.

**POETRY**
1. Poets of Africa: Lament of silent by Jared Angira & other poems

**LITERATURE IN ENGLISH (For HGLi)**

**NOVELS.**
1. A Grain of Wheat by Ngugi wa Thiong'o
2. No Longer at Ease by Chinua Achebe.

**PLAYS**
1. Julius Ceasar by William Shaka Speare.
2. Man of Kafira by Francis Imbuga.

**POETRY**
1. Poets of Africa Boundles by Arthur I Luvai Voice: Poem from Kenya.

**ACADEMIC COMMUNICATION**

**1.** Academic Communication For Advanced Secondary Schools, Student's Book Form Five.

2. Academic Communication Communication For advanced Secondary Schools, Student's Book Form Six.

**CHEMISTRY**

**1.** General Chemistry For Advanced Level – TIE (New Syllabus 2025)
2. Physical Chemistry for Advanced Level – TIE (New Syllabus 2025)
3. Organic Chemistry for Advance Level - TIE ( New Syllabus 2025)
4. Essentials of Physical Chemistry Chemistry by S. Chand.
5. A level Chemistry 4$^{th}$Ed- by S.K Jain.
6. Cconceptual Chemistry for class XII – by S. Chand.
7. General Chemistry by APE.

ECONOMICS.
1. Microeconomics for Advanced Secondary Schools by TIE.
2. Macroeconomics for Advanced Secondary Schools by TIE.
3. Microeconomics and Macroeconomics (New Curriculum) by a. A Othiambo
b. Mwakagile
c. Sir Ally
d. Zist Kamili.
4. Simplified Fundamentals of economics; F V and VI by Sir Ally.

KISWAHILI
**VITABU VYA WANAFUNZI WA HKL**
1. Dunia Uwanja wa Fujo – Euphase Kezilahabi.
2. Ua la Faraja – W.E Nkufya.
3. Mirathi ya Hatari – C-G Nung'ong'o.
4. Wasifu wa Binti Saad- Shaban Robert

**TAMTHILIYA**
1. Mukwawa wa Uhehe – M.M Mulokozi
2. Shujaa wa Milambo – E Mbogo
3. Usaliti Mjini – Francis Imbuga

**USHAIRI**

**1.** Fumbo linaloelea – Nyambari Nyangwine
2. Malengo wazi Wakuu – Walah Bin Wallah.
3. Andamo Msafiri Safarini – Mohammed K. Ghassani
4. Wosia wa Baba – Ahmed Mohamed Amany.

VITABU VYA WANAFUNZI WA HGFa RIWAYA

1. Vuta N'kuvute – Shafi Adam Shafi
2. Asali Chngu – Said Ahmed Mohamed.
3. Mama wa Yagi Hulewa – Mohamed Said Abdula.
4. Vipuli Figo – Emanuel Mbogo.

Tamthiliya
1. Kaptula la Max – Euphrase Kezilahabi.
2. Nyerere na safari ya Kanaani – Emanuel Mbogo.
3. Morani – Emanuel Mbogo.

Ushairi.
1. Dhifa – Euphrase Kezilahabi.
2. Utenzi Masumuiwa Karne ya 21 – Idd M Mwimbe.
3. Malenga wa Bara - M.M Mulokozi
4. Fungate ya Uhuru – Mohamed Seif Khatibu.

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

Historia ya Tanzania na maadili kidato cha Tano - TIE